

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

HOTUBA YA MKURGENZI MTENDAJI WILAYA YA MPWAPWA NDUGU PAUL MAMBA SWEYA KWENYE MAFUNZO YA KAMATI YA WILAYA YA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU TAREHE 31/08/2018.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma

kwa Watu Wenye Ulemavu wilaya ya Mpwapwa

Mratibu wa Mradi na Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Mkoa wa Dododma

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana (W) ya
Mpwapwa

Ndugu Wajumbe wenzangu

Muwezesaji wa Mafunzo

Ndugu wageni waalikwa, Mabibi na mabwana

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha Siku hii ya leo. Pia napenda kuwapongeza wajumbe wote pamoja na mimi kwa kupata bahati ya kuunda au kuanzisha Kamati hii mpya ya toka ilipoanzishwa Sheria Na.9 ya mwaka 2010 ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

Aidha, napenda kuwashukuru sana na kuwapongeza ninyi wajumbe mlioitikia wito wa kuhudhuria mafunzo haya nafahamu baadhi yenu mnatoka nje ya Mji wa Mpwapwa.

Shukrani za kipekee ziwaendee Chama cha Wasioona Tanzania Mkoa wa Dodoma kwa kuona umuhimu wa kupata angalao siku mbili za kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Watu Wenye Ulemavu ya Wilaya, nafahamu raslimali ni chache lakini wameoona si vyeme kuwa na Kamati

ambayo itaanza kutekeleza majukumu yake bila ya kuelewa Sheria iliyounda Kamati hii muhimu kwa usimamizi na maendeleo ya ustawi wa watu wenye ulemavu.

Ndugu Wajumbe,

Kamati hii ina majukumu mengi na makubwa katika kuboresha ustawi na maendeleo ya watu wenye ulemavu, hivyo pamoja na majukumu mengi tuliyonayo niwaombe mtumie muda wetu mwingi kuhakikisha ndugu zetu hawa wanapata huduma stahili kama wale wasio na ulemavu wanazipata. Tukumbuke kuwa sisi sote ni walemavu watarajiwa kwani wale wenye ulemavu hawakuumbwa wawe walemavu.

Najua kwenye mafunzo haya tutapata muda wa kujua mengi juu ya Sheria inayohudumia watu wenye ulemavu pia majukumu ya Kamati, kwa kifupi Kamati yetu ina majukumu yafuatayo:

- i. Kutekeleza maelekezo mbalimbali kuhusiana na watu wenye ulemavu katika wilaya
- ii. Kuratibu shughuli zote za watu wenye ulemavu katika wilaya
- iii. Kulinda na kuendeleza masuala yote yanayohusiana na ustawi na maendeleo ya watu wenye ulemavu katika wilaya
- iv. Kupokea taarifa za utekelezaji za vipindi mbalimbali toka kwenye Kamati za Vijiji au Mitaa
- v. Kuwasilisha taarifa za kina za robo mwaka kwa Kamati ya Watu Wenye Ulemavu Mkoa
- vi. Kupokea na kuamua malalamiko kuhusiana na Watu Wenye Ulemavu
- vii. Kutunza kumbukumbu sahihi za vikao vya Kamati

viii. Kutunza takwimu au rejesta ya watu wenye ulemavu kwenye eneo la Halmashauri.

Hivyo mtaona tulivyo na kazi kubwa ya kuwahudumia watu wenye Ulemavu ikizingatiwa kuwa majukumu haya ni ya kujitolea hivyo tunatakiwa kujizatiti sana ili malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. John Pombe Joseph Magufuli kwa Watu wenye Ulemavu yaweze kutimia.

Ndugu Wajumbe,

Mafunzo haya yatatusaidia kuifahamu vyema Sheria ya Watu wenye ulemavu ambayo toka ilipoanzishwa mwaka 2010 kwanza ilikuwa haifahamiki kwa jamii, kwa watekelezaji na hata kwa Watu wenye ulemavu wenyewe.

Serikali kwa upande wake itaendelea kuisimamia Sheria hii kwa kuondoa na kutimiza mahitaji stahili ya Watu wenye ulemavu, miundo mbinu inayojengwa kama vile shule, zahanati, Vituo vya Afya, majengo ya biashara, masoko na utoaji wa mikopo kwa ajili ya wanawake na vijana walemavu yanapatiwa kipaumbele ambapo Halmashauri ya Wilaya Katika bajeti yake kwa mwaka 2018/19 imetenga asilimia 2 kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.

Pia tutahakikisha Kamati za Huduma kwa Watu wenye ulemavu na Mahitaji Maalum kwenye ngazi zote za utawala za vijiji na Kata zinaundwa baada ya Kamati ya Wilaya kuanza kazi. Wilaya itaweka utaratibu wa namna ya kutekeleza shughuli za Watu Wenye Ulemavu kwa ngazi zilizotajwa ili kuwezesha upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa watu hao.

Halmashauri ya Wilaya itaboresha daftari la Watu Wenye Ulemavu na Wenye mahitaji Maalum ili kuwa na kumbukumbu sahihi za walemavu wote.

Ndugu wajumbe,

Mwisho naomba niwashukuru tena kwa kukubali kutekeleza jukumu hili zito la Kamati ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na kwa kukubali kuhudhuria mafunzo haya ambayo yatatupa mwanga wa kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Baada ya kusema haya **nitamke rasmi kuwa mafunzo yetu ya kuijengea uwezo Kamati juu ya Sheria Na.9 ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 yamefunguliwa rasmi.**

Mungu Watu Wote Wenye Ulemavu

Mungu Ibariki Mpwapwa

Mungu Ibariki Tanzania

Ahsanteni Sana kwa Kunisikiliza.